**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS–TAMISEMI**

**MPUI SHULE YA SEKONDARI,**

**S.L.P 338 SUMBAWANG.A**

**Tarehe...................…………….**

**Namba za Simu:-**

**Mkuu wa Shule: 0758432825**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0765817243**

**Matron: 0758063445**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………...............................**
**S.L.P……………………………………..**
**…………………………………………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya …….

Shule ya Sekondari MPUI ipo umbali wa Kilometa 55 Mashariki mwa Mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi **Katumba** na nauli ni Shilingi 3,000/=. Kwa usafiri wa hiace zinazoelekea mji Mdogo wa Laela. Aidha kwa wale wanaotokea barabara ya Mbeya-Sumbawanga unapaswa kushuka kituo cha **Mpui ya UFIPA Ambapo shule ipo mita TANO TU toka barabara kuu**.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe**…………,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………., Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**(a) Sare za Shule**

(i) Sare ya shule hii ni sketi mbili, Moja ya kijani iliyoiva (kitambaa kizito) na moja ya zambarau iliyoiva (kitambaa kizito). Sketi iwe ndefu inayofika chini na kugusa viatu. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.

(ii) Tai moja ya kijani iliyoiva na moja ya zambarau iliyoiva.

(iii) Rangi ya hijabu (kijuba) iwe nyeupe tu na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

(iv) Sare ya Michezo kwa shule hii ni track suti rangi ya bluu bahari na raba za michezo jozi Moja.

(v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(vi) Soksi jozi mbili nyeupe

(vii) Masweta mawili moja la kijani iliyoiva na moja la zambarau iliyoiva.

(viii) Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni magauni mawili mshono wa solo (bajaji) rangi ya pinki na iwe ndefu mpaka kifundo cha mguu.

(ix) Aje na Tisheti (T-shirt) yenye kora (Form six) rangi ya bluu isiyo kolea ( light blue.)

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya maelekezo hapo juu na siku ya kuripoti avae sare za shule.

**(b) Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shule ni:-**

i. Madaftari counter books 7 (3 quire)
ii. **Ream(A4)** Mbili aina ya **paperline** (2) kwa mwaka;
iii. Godoro moja.
iv. Mashuka mawili rangi ya pink,blanketi moja na chandarua
v. Nguo za ndani za kutosha
vi. Aje na vyombo vya kulia chakula kama ; Bakuli lenye mfuniko,kijiko, na kikombe

(c) vifaa vya usafi

i. Ndoo moja ya lita kumi
ii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio wa chelewa mmoja

**(c) Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Michango hii ilipwe kwenye akaunti 62102300244 MPUI SECONDARY SCHOOL.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizaraya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada yakuripoti shuleni. Mambo hayoni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) passport size za mwanafunzi.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**

**Pudensiana John Kambole.**
Mkuu wa shule

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NIVEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuuwashule - 0758432825**
- **Makamu Mkuu wa Shule - 0765817243**
- **Mwandamizi Malezi - 0758063445**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA**
**SHULE YA SEKONDARI MPUI**

## FOMU YA MKATABA

Unatakiwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu.

### SEHEMU A: MWANAFUNZI

Mimi…………………………………………………………nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote za shule, **nakubali/sikubali** nafasi hii na kwa uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii sheria, maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

Saini………………………………………..

Tarehe……………………………………….

### SEHEMU B: MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………………………………………..Mzazi/Mlezi wa………………………………………………. Nimepokea taarifa ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari MPUI. Kwa kutambua umuhimu wa taaluma na wajibu wangu, naahidi kuwa, muda wote mwanangu atakapo kuwa shuleni nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea mtoto kwa kufuata sheria, maagizo na kanuni zote za shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule. Nitatekeleza yote yatakayo tolewa na shule na nitatoa kwa wakati michango yote ya shule iliyo idhinishwa na Wizara ya Elimu ,Sayansi na Teknolojia na itakayo afikiwa baina ya wazazi na shule.

Saini……………………………………………..
Tarehe………………………………………….

**SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL**
**MPUI HIGH SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officer in respect to all form of entrants

Student's full name………………………………………………………………………

Age……………………………… Years……………………………………. Sex

Blood count (red and white)
…………………………………………………………………………………………………

Stoolexamination…………………………………………………………………………………

Urine analysis, syphilis and other venereal disease test……………………………………………

T.B test…………………………………………………………………………………………

Eye test…………………………………………………………………………………………

Ears………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………..

Abdomen…………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

Urine for plant test……………………………………………………………………………….

Test for pregnancy……………………………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION**

Defects, impotent (e.g. arms, legs etc.) infections, chronic or family disease etc.

…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..…

…………………………………………………………………………………………………

I certify that the named above is fit to pursue further studies and domestic education

Station……………………………………………………………..……………….
Signature……………………………………………………………………………….

Date………………………………………………………………………..…….
Designation……………………………………………………………………………….

**SHULE YA SEKONDARI MPUI – SUMBAWANGA**
**FOMU YA KUANDIKISHA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

Jina kamili……………………………………………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………………………

Dini…………………………………………………………………………………………………

Uraia ……………………………………………………………………………………..

Anwani ya nyumbani…………………………………………………………………
Simu ya babaMzazi/baba mlezi………………………………………………………………….
Simu ya mama/ mama mlezi……………………………………………………………..

Simu ya mtendaji wa mtaa au Kijiji………………………………………………………………

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU AFYA YA MWANAFUNZI**

…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..…

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………

Nathibitisha kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni **kamili na kweli.**
Sahihi baba/mama/mlezi